BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA

# UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WATAHINIWA KATIKA MASWALI YA MTIHANI WA KUMALIZA ELIMU YA MSINGI MWAKA 2012

# KISWAHILI

# BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA

# UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WATAHINIWA KATIKA MASWALI YA MTIHANI WA KUMALIZA ELIMU YA MSINGI MWAKA 2012

## KISWAHILI

Kimechapishwa na
Baraza la Mitihani la Tanzania,
S.L.P. 2624,
Dar es Salaam, Tanzania.

© Baraza la Mitihani la Tanzania, 2013

Haki zote zimehifadhiwa.

# YALIYOMO

DIBAJI ........................................................................................................................iv
1.0 UTANGULIZI................................................................................................1
2.0 UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WATAHINIWA...........................................1
2.1 Sehemu A: Sarufi ........................................................................................1
2.2 Sehemu B: Lugha ya Kifasihi......................................................................14
2.3 Sehemu C: Ufahamu ..................................................................................20
2.4 Sehemu D: Ushairi .....................................................................................27
2.5 Sehemu E: Utungaji....................................................................................31
3.0 HITIMISHO..................................................................................................32
4.0 MAONI NA MAPENDEKEZO .....................................................................33

# DIBAJI

Taarifa ya uchambuzi wa majibu ya maswali ya Mtihani wa Kumaliza Elimu ya Msingi kwa somo la Kiswahili imeandaliwa kwa lengo la kutoa mrejesho kwa wanafunzi, walimu, watunga sera, wakaguzi, watunga mitaala na wadau wengine wa elimu kuhusu namna wanafunzi walivyojibu maswali ya mtihani huo. Majibu ya wanafunzi katika mtihani ni kiashiria kimojawapo kinachoonesha mambo ambayo wanafunzi waliweza kujifunza kwa ufasaha na yale ambayo hawakuweza kujifunza kwa ufasaha katika kipindi cha miaka saba ya elimu ya msingi.

Katika taarifa hii, mambo mbalimbali ambayo yamechangia watahiniwa kushindwa kujibu maswali kwa usahihi yameainishwa. Uchambuzi unaonesha kuwa yafuatayo yamechangia kuwafanya wanafunzi kutoweza kujibu maswali kwa usahihi: Kushindwa kutambua matakwa ya swali; kuwa na uelewa mdogo wa mada mbalimbali katika somo; kutofahamu kanuni za lugha na matumizi ya misamiati; kutojibu kabisa baadhi ya maswali au kuchagua jibu zaidi ya moja kinyume na maelekezo katika mtihani. Uchambuzi kwa kila swali umefanyika ambapo dosari mbalimbali zilizojitokeza wakati watahiniwa walipokuwa wanajibu maswali yao zimeainishwa kwa kuonesha idadi ya watahiniwa waliojibu maswali kwa usahihi, walioshindwa kuchagua jibu sahihi, waliaocha kujibu swali na ambao waliandika jibu zaidi ya moja katika swali husika.

Baraza la Mitihani la Tanzania lina imani kuwa mrejesho uliotolewa utawawezesha wadau mbalimbali wa elimu kuchukua hatua madhubuti ili kuboresha ufundishaji na ujifunzaji kwa lengo la kupatia ufumbuzi dosari zilizoainishwa katika taarifa hii. Aidha, Baraza la Mitihani la Tanzania lina imani kuwa endapo maoni yaliyotolewa yatafanyiwa kazi ipasavyo, ujuzi na maarifa watakayopata wanafunzi wanaohitimu elimu ya msingi vitaongezeka na hatimaye kiwango cha ufaulu katika Mtihani wa Kumaliza Elimu ya Msingi kitaongezeka pia.

Mwisho Baraza la Mitihani linapenda kutoa shukrani za dhati kwa Maafisa Mitihani, Makatibu Muhtasi na wengine wote waliohusika katika kuandaa taarifa hii. Baraza litashukuru kupokea maoni na mapendekezo kutoka kwa walimu, wanafunzi na wadau wengine wa elimu kwa ujumla ambayo yatasaidia katika kuboresha taarifa ya uchambuzi wa maswali ya Mtihani wa Kumaliza Elimu ya Msingi kwa siku zijazo.



Dkt. Joyce L. Ndalichako
**KATIBU MTENDAJI**

## 1.0 UTANGULIZI

Taarifa hii imeandaliwa kwa lengo la kutoa mrejesho kuhusu namna ambavyo watahiniwa walijibu maswali katika mtihani wa somo la Kiswahili. Mtihani wa Kiswahili ulikuwa na maswali **50** ya kuchagua jibu sahihi ambayo yalikuwa yamegawanywa katika sehemu tano kama ifuatavyo: Sehemu A: Sarufi; B: Lugha ya Kifasihi; C: Ufahamu; D: Ushairi; na E: Utungaji. Jumla ya watahiniwa **865,173** walifanya mtihani wa somo la Kiswahili na kati yao watahiniwa **354,588** sawa na asilimia **41.0** walifaulu mtihani huo.

## 2.0 UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WATAHINIWA

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa kwa kila swali umefanyika na sehemu hii inaainisha maswali yaliyoulizwa kwa watahiniwa na majibu ya kuchagua waliyopewa. Aidha idadi ya watahiniwa waliochagua kila jibu na asilimia yao imeoneshwa na uchambuzi wa sababu zinazoweza kuwa zilichangia kuwafanya wasichague jibu sahihi zimeainishwa.

### 2.1 Sehemu A: Sarufi

**Swali la 1**: Katika maneno yafuatayo ni lipi ambalo ni nomino dhahania?

A. Unakuja
B. Umeenea
C. Utalima
D. Uelewa
E. Ulisoma.

Majibu ya watahiniwa

| Chaguo | A | B | C | D* | E | Wasiojibu | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya watahiniwa** | 225,612 | 149,888 | 165,634 | 187,841 | 127,507 | 6,509 | 2,115 |
| **Asilimia ya watahiniwa** | 26.08 | 17.33 | 19.15 | 21.71 | 14.74 | 0.75 | 0.24 |

Swali la 1 lililenga kupima uwezo wa mtahiniwa wa kutambua aina za nomino. Asilimia 21.71 ya watahiniwa walichagua jibu D ambalo ndilo jibu sahihi. Asilimia 26.08 ya watahiniwa walichagua kipotoshi A ambacho ni kitenzi cha wakati uliopo. Watahiniwa hao walipotoshwa na umbo -U- ambalo katika kitenzi "Unakuja" umbo hilo linaonesha nafsi ya pili umoja. Hali kadhalika kuwepo kwa asilimia 17.33 ya watahiniwa waliochagua kipotoshi B "Umeenea" ambacho ni kitenzi katika wakati timilifu; asilimia 19.15 kipotoshi C "Utalima" ambacho ni

kitenzi kilichopo katika wakati ujao; na asilimia 14.74 waliochagua E “Ulisoma” ambacho ni kitenzi katika wakati uliopita kunaonesha wazi kuwa watahiniwa hao hawakuwa na ujuzi kuhusu dhana ya nomino dhahania. Watahiniwa walipotoshwa na umbo -U- lililojitokeza katika kila neno hivyo kuwafanya washindwe kutofautisha kuwa katika vitenzi umbo hili hutumika kuwakilisha nafsi ya pili umoja na upatanisho wa ngeli.

**Swali la 2**: Wingi wa neno paka ni upi?

A. Mipaka
B. Paka
C. Mapaka
D. Vipaka
E. Wapaka.

Majibu ya watahiniwa

| Chaguo | A | B* | C | D | E | Wasiojibu | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Idadi ya watahiniwa | 110,545 | 539,901 | 153,023 | 39,698 | 18,419 | 1,643 | 1,877 |
| Asilimia ya watahiniwa | 12.78 | 62.41 | 17.69 | 4.59 | 2.13 | 0.19 | 0.22 |

Swali lililenga kupima uwezo wa mtahiniwa kutumia maneno katika umoja na wingi. Watahiniwa walio wengi walikuwa na uelewa wa swali hili kwani asilimia 62.41 walichagua jibu B ambalo ni sahihi. Uchaguzi wa kipotoshi A “Mipaka” kwa watahiniwa 110,545 ambao ni sawa na asilimia 12.78 unaonesha kuwa watahiniwa hao waliathiriwa na tabia ya baadhi ya nomino ambazo zina uwezo wa kupokea umbo la wingi, kwa mfano mti (umoja) na miti (wingi). Uchaguzi wa kipotoshi C “Mapaka” kwa asilimia 17.69 ya watahiniwa unaonesha kuwa waliweka neno “Paka” katika kundi la nomino zenye umbo la Ma- katika wingi, kwa mfano Dawati- Madawati. Uchaguzi wa kipotoshi D na E unaonesha kuwa watahiniwa hawakuwa na ujuzi wa kutosha kuhusu wingi wa nomino. Hali hii inadhihirisha wazi kuwa watahiniwa hudhani kuwa kila neno likiwa katika wingi ni lazima umbo la neno libadilike yaani kuwepo na umbo mahsusi la kuonesha wingi.

**Swali la 3**: “Akiondoka Sulubu kazi zote zitalala.” Neno sulubu ni la aina gani?

A. Kielezi
B. Kivumishi
C. Kiwakilishi
D. Nomino
E. Kiunganishi.

Majibu ya watahiniwa

| Chaguo | A | B | C | D* | E | Wasiojibu | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya watahiniwa** | 178,531 | 157,607 | 174,393 | 264,076 | 83,705 | 4,173 | 2,621 |
| **Asilimia ya watahiniwa** | 20.64 | 18.22 | 20.16 | 30.53 | 9.68 | 0.48 | 0.3 |

Swali lililenga kupima ujuzi wa aina za maneno na lilimtaka mtahiniwa kutambua neno Sulubu limetumika kama aina gani ya neno katika tungo hiyo. Asilimia 30.53 ya watahiniwa walichagua jibu D "Nomino" ambalo ni jibu sahihi. Uchaguzi wa kipotoshi A "Kielezi" ambao ni asilimia 20.64 unaonesha kuwa watahiniwa walivutiwa na dhana ya kuwa neno linalofuatana na kitenzi ni kielezi hata kama halitoi taarifa kuhusu kitenzi hicho. Kuwepo kwa jumla ya asilimia 48.06 ya waliochagua vipotoshi B, C na E kunaonesha wazi kuwa watahiniwa walikosa ujuzi wa sintaksia ya Kiswahili ambayo inaonesha mpangilio wa maneno katika tungo. Aidha, watahiniwa hao walionekana kukosa ujuzi wa kutambua aina za maneno zikiwemo nomino za pekee ambazo zinapoandikwa huanza na herufi kubwa hata kama ni neno lililo katikati ya maneno mengine.

**Swali la 4**: "Ili tuendelee________ kufanya kazi kwa bidii." Neno lipi limekosekana kukamilisha sentensi hiyo?

A. ni budi
B. hatuna budi
C. tuna budi
D. kuna budi
E. hapana budi.

Majibu ya watahiniwa

| Chaguo | A | B* | C | D | E | Wasiojibu | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya watahiniwa** | 149,377 | 376,777 | 233,263 | 48,370 | 52,524 | 2,284 | 2,511 |
| **Asilimia ya watahiniwa** | 17.27 | 43.55 | 26.96 | 5.59 | 6.07 | 0.26 | 0.29 |

Swali lililenga kupima matumizi ya msamiati wa Kiswahili ambapo ni asilimia 43.55 tu ya watahiniwa ndio waliochagua jibu B "hatuna budi" ambalo ndilo jibu sahihi. Asilimia 26.96 walichagua jibu C "tuna budi" ambalo si jibu sahihi. Watahiniwa hao walipotoshwa na dhana ya uyakinishi iliyopo katika sentensi wakati jibu sahihi linaonekana kuwa na dhana ya ukanushi. Aidha, uchaguzi

wa vipotoshi A, D na E unaonesha kuwa watahiniwa hawakuwa na ujuzi wa sarufi ya Kiswahili kwani sentensi ipo katika nafsi ya kwanza wingi lakini vipotoshi hivyo havina dhana yoyote inayorejea nafsi.

**Swali la 5**: "Mvua ilinyesha jana usiku kucha." Katika sentensi hiyo kikundi kielezi ni kipi?

A. Mvua ilinyesha jana
B. Usiku kucha
C. Ilinyesha jana
D. Mvua ilinyesha
E. Jana usiku kucha.

Majibu ya watahiniwa

| **Chaguo** | **A** | **B** | **C** | **D** | **E*** | **Wasiojibu** | **Mengine** |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya watahiniwa** | 279,839 | 220,363 | 102,716 | 118,639 | 136,955 | 3,640 | 2,954 |
| **Asilimia ya watahiniwa** | 32.35 | 25.47 | 11.87 | 13.71 | 15.83 | 0.42 | 0.34 |

Swali lililenga kupima uwezo wa watahiniwa kutumia sarufi ya lugha. Swali hili ni mojawapo kati ya maswali ambayo hayakufanyika vizuri kwani ni asilimia 15.83 tu ya watahiniwa ndio waliochagua jibu sahihi ambalo ni E "Jana usiku kucha". Uchaguzi wa vipotoshi A, C na D unaonesha kuwa watahiniwa hawakuwa na ujuzi wa vikundi vielezi katika lugha, kwani vipotoshi hivyo vina kitenzi "ilinyesha" ambacho si kielezi. Uchaguzi wa kipotoshi B "Usiku kucha" unaonesha kuwa watahiniwa walikosa ujuzi wa sintaksia ya Kiswahili ambao ni mpangilio wa maneno katika tungo. Neno jana ni kielezi cha wakati ambapo tendo hili lilitokea, hivyo kukosekana kwa neno hilo kunasababisha kipotoshi B kutokuwa jibu sahihi. Licha ya kuwepo kwa asilimia ndogo ya watahiniwa waliojibu swali hilo kwa usahihi, jumla ya watahiniwa 3,640 hawakujibu kabisa swali hilo na watahiniwa 2,954 walichagua jibu zaidi ya moja kinyume na maelekezo. Hali inayoonesha kuwa mada ya sarufi ya lugha haikuwa imeeleweka vizuri kwa watahiniwa walio wengi.

**Swali la 6**: "Baba alilimiwa shamba." Sentensi hii ipo katika kauli gani?

A. Kutenda
B. Kutendewa
C. Kutendwa
D. Kutendeka
E. Kutendea.

Majibu ya watahiniwa

| Chaguo | A | B* | C | D | E | Wasiojibu | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya watahiniwa** | 58,855 | 635,482 | 78,273 | 55,716 | 32,336 | 1,970 | 2,474 |
| **Asilimia ya watahiniwa** | 6.8 | 72.46 | 9.05 | 6.44 | 3.74 | 0.23 | 0.29 |

Swali lililenga kupima ujuzi wa kauli za vitenzi. Swali hili ni miongoni mwa maswali yaliyojibiwa kwa usahihi na idadi kubwa ya watahiniwa katika mtihani huu ambapo asilimia 72.46 walichagua jibu sahihi B "kutendewa". Sababu iliyowafanya watahiniwa kupata swali hili kwa usahihi ni uwezo wa kuhusisha umbo la kisarufi -ew- lililopo katika kauli ya kutendewa na -iw- lililopo katika kitenzi "alilimiwa". Watahiniwa wachache waliochagua kati ya vipotoshi A, D na E ambao ni asilimia 16.98 walishindwa kugundua upungufu uliokuwepo katika vipotoshi hivyo ambapo umbo –iw- linakosekana. Aidha waliochagua kipotoshi C ambao ni asilimia 9.05 walivutiwa na umbo la –w- bila kujua kuwa umbo hili lipo katika kauli ya kutendwa na wala sio kutendewa.

**Swali la 7**: "Adili alikuwa anaimba tangu ujana wake". Neno "alikuwa" ni aina gani ya kitenzi?

A. Kisaidizi
B. Jina
C. Kishirikishi
D. Kitegemezi
E. Kikuu.

Majibu ya watahiniwa

| Chaguo | A* | B | C | D | E | Wasiojibu | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya watahiniwa** | 28,5548 | 90,652 | 226,775 | 128,114 | 127,261 | 3,903 | 2,853 |
| **Asilimia ya watahiniwa** | 33.01 | 10.48 | 26.21 | 14.81 | 14.71 | 0.45 | 0.33 |

Swali lililenga kupima uwezo wa mtahiniwa wa kutambua aina za vitenzi vya Kiswahili. Asilimia 33.01 ya watahiniwa walichagua jibu A "Kisaidizi" ambalo ni jibu sahihi. Asilimia 26.21 walichagua kipotoshi C "Kishirikishi" ambacho si jibu sahihi. Uchaguzi wa kipotoshi hicho unaonesha jinsi watahiniwa walivyoshindwa kutofautisha dhana ya kitenzi kisaidizi na kitenzi kishirikishi. Hali kadhalika watahiniwa walishindwa kutambua mpangilio sahihi wa maneno katika tungo. Kitenzi kisaidizi hutokea kabla ya kitenzi kikuu na ndio maana

neno “alikuwa” ambalo ni kitenzi kisaidizi limetokea kabla ya neno “anaimba” ambalo ni kitenzi kikuu. Katika kanuni za lugha ya Kiswahili, kitenzi kishirikishi hakiwezi kuwa sambamba na kitenzi kingine cha aina yoyote. Hivyo uchaguzi wa vipotoshi B, D na E unadhihirisha kuwa watahiniwa hao hawakuwa na ujuzi wa kutosha kuhusu dhana ya vitenzi visaidizi.

**Swali la 8:** “Mchungaji alivaa suti maridadi sana.” Katika sentensi hii ni neno lipi limetumika kama kivumishi?

A. Suti
B. Alivaa
C. Maridadi
D. Mchungaji
E. Sana.

Majibu ya watahiniwa

| Chaguo | A | B | C* | D | E | Wasiojibu | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya watahiniwa** | 131,752 | 177,782 | 333,716 | 98,501 | 117,607 | 2,908 | 2,840 |
| **Asilimia ya watahiniwa** | 15.23 | 20.55 | 38.58 | 11.39 | 13.59 | 0.34 | 0.33 |

Swali lililenga kupima ujuzi wa watahiniwa kuhusu aina za maneno na hasa dhana ya kivumishi. Ni asilimia 38.58 tu ya watahiniwa waliofanya mtihani ndio waliochagua jibu sahihi ambalo ni C “Maridadi”. Uteuzi wa vipotoshi A na D unadhihirisha kuwa watahiniwa walikosa ujuzi wa kutosha kuhusu dhana ya kivumishi kwani vipotoshi hivyo ni nomino na sio vivumishi. Aidha uchaguzi wa kipotoshi E ambao ulifanywa na asilimia 13.59 ya watahiniwa unaonesha kuwa walishindwa kuelewa kuwa neno “sana’ ni kielezi kwavile limetumika kutoa taarifa zaidi kuhusu kivumishi “maridadi.” Asilimia 20.55 ya watahiniwa walichagua jibu B ”Alivaa” ambalo si jibu sahihi. Hali hiyo inaonesha wazi kuwa watahiniwa hao walishindwa kuelewa matakwa ya swali, kwani neno “alivaa” linajidhihirisha wazi kuwa ni tendo na hivyo haliwezi kuwa kivumishi.

**Swali la 9:** Kitenzi “anapigwa” kipo katika kauli gani?

A. Kutenda
B. Kutendewa
C. Kutendwa
D. Kutendeka
E. Kutendesha.

Majibu ya watahiniwa

| Chaguo | A | B | C* | D | E | Wasiojibu | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya watahiniwa** | 80,551 | 243,989 | 414,353 | 89,619 | 31,618 | 2,618 | 2,358 |
| **Asilimia ya watahiniwa** | 9.31 | 28.2 | 47.9 | 10.36 | 3.65 | 0.3 | 0.27 |

Swali lililenga kupima maarifa ya mtahiniwa kuhusu dhana ya utendwa. Asilimia 47.9 ya watahiniwa waliweza kuchagua jibu sahihi ambalo ni C “Kutendwa”. Watahiniwa waliochagua A, D na E walishindwa kuhusisha dhana ya utendwa na umbo -W- lililopo katika kitenzi anapigwa. Aidha watahiniwa waliochagua kipotoshi B “Kutendewa” ambao ni asilimia 28.2 walivutiwa na umbo la –ew- na kulihusisha na dhana ya utendwa wakati neno hilo lipo katika dhana ya utendewa.

**Swali la 10:** Kisawe cha neno “bahati” ni kipi kati ya maneno yafuatayo?

A. Tunu
B. Sudi
C. Shani
D. Hiba
E. Hidaya.

Majibu ya watahiniwa

| Chaguo | A | B* | C | D | E | Wasiojibu | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya watahiniwa** | 195,815 | 159,724 | 148,006 | 165,142 | 186,217 | 7,356 | 2,846 |
| **Asilimia ya watahiniwa** | 22.63 | 18.46 | 17.11 | 19.09 | 21.53 | 0.85 | 0.33 |

Swali lililenga kupima uwezo wa mtahiniwa katika kutumia msamiati. Ni asilimia 18.46 tu ya watahiniwa waliofanya mtihani waliweza kuchagua jibu sahihi ambalo ni B “Sudi”. Asilimia 22.63 ya watahiniwa walichagua A ambalo si jibu sahihi. Watahiniwa hawa walishindwa kutofautisha neno bahati na neno tunu ambalo maana yake ni zawadi, na wala si bahati. Aidha, inawezekana watahiniwa walichanganya suala la kupewa tunu (kuzawadiwa) na kuwa na bahati kwa kudhani kuwa wanaotunukiwa ni wale wenye bahati na hivyo kushindwa kutofautisha maneno hayo.

Kwa ujumla majibu yaliyotolewa katika swali la 10 yanaonesha wazi kuwa watahiniwa hawakuwa na ujuzi wa kutosha wa msamiati wa Kiswahili kwa vile vipotoshi A, D na E vina maana moja ambayo ni kama zawadi. Swali hili ni miongoni mwa maswali ambayo watahiniwa wengi hawakujibu kabisa kama inavyoonekana kwenye jedwali ambapo watahiniwa 7,356 hawakulijibu wakati watahiniwa 2,846 walichagua jibu zaidi ya moja.

**Swali la 11:** "Maandishi yanasomeka vizuri." Sentensi hii ipo katika wakati gani?

A. Ujao
B. Uliopita
C. Mazoea
D. Uliopo
E. Timilifu

Majibu ya watahiniwa

| Chaguo | A | B | C | D* | E | Wasiojibu | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya watahiniwa** | 45,626 | 66,082 | 62,107 | 560,295 | 125,398 | 2,943 | 2,655 |
| **Asilimia ya watahiniwa** | 5.27 | 7.64 | 7.18 | 64.77 | 14.5 | 0.34 | 0.31 |

Swali lililenga kupima uwezo wa mtahiniwa katika kutumia njeo ya wakati. Asilimia 64.77 walichagua D "Uliopo" ambalo ni jibu sahihi kwa kuwa kitenzi "yanasomeka" kina umbo "–na-" ambalo ni umbo la wakati uliopo. Uteuzi wa vipotoshi A, B, C na E unaonesha jinsi watahiniwa husika walivyoshindwa kutambua maumbo yanayowakilisha dhana mbalimbali za njeo katika sarufi ya Kiswahili.

**Swali la 12:** "Makubi ni mtoto wa mjukuu wangu". Makubi ni nani kwangu?

A. Kilembwekeza
B. Kijukuu
C. Kilembwe
D. Kitukuu
E. Mtukuu.

Majibu ya watahiniwa

| Chaguo | A | B | C | D* | E | Wasiojibu | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya watahiniwa** | 99,630 | 123,884 | 177,482 | 403,402 | 54,683 | 3,484 | 2,541 |
| **Asilimia ya watahiniwa** | 11.52 | 14.32 | 20.52 | 46.63 | 6.32 | 0.4 | 0.29 |

Swali lililenga kupima ujuzi wa mtahiniwa kuhusu matumizi ya msamiati unaoonesha uhusiano wa watu katika jamii. Asilimia 46.63 ya watahiniwa walichagua jibu D "Kitukuu" ambalo ni jibu sahihi. Uchaguzi wa vipotoshi A, B, C na E ulidhihirisha kuwa baadhi ya watahiniwa walikuwa hawajui msamiati sahihi unaoelezea uhusiano wa kindugu katika jamii.

**Swali la 13:** "Sipendi uongo". Sentensi hii ipo katika nafsi ipi?

A. Nafsi ya kwanza wingi
B. Nafsi ya tatu umoja
C. Nafsi ya kwanza umoja
D. Nafsi ya tatu wingi
E. Nafsi ya pili umoja.

Majibu ya watahiniwa

| Chaguo | A | B | C* | D | E | Wasiojibu | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya watahiniwa** | 162,544 | 111,363 | 397,177 | 65,331 | 122,062 | 3,722 | 2,907 |
| **Asilimia ya watahiniwa** | 18.79 | 12.87 | 45.91 | 7.55 | 14.11 | 0.43 | 0.34 |

Swali lililenga kupima ujuzi wa mtahiniwa katika sarufi ya lugha. Asilimia 45.91 ya watahiniwa walichagua C "Nafsi ya kwanza umoja" ambalo ni jibu sahihi. Uchaguzi wa vipotoshi A, B, D na E unadhihirisha kuwa watahiniwa hawakuwa na ujuzi wa kutosha kuhusu matumizi ya maumbo yanayowakilisha nafsi mbalimbali.

**Swali la 14:** Neno "poni" lina maana sawa na neno lipi kati ya maneno yafuatayo?

A. Posho
B. Rahani
C. Mali
D. Mkopo
E. Pesa.

Majibu ya watahiniwa

| Chaguo | A | B* | C | D | E | Wasiojibu | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya watahiniwa** | 279,172 | 185,838 | 113,428 | 199,496 | 77,401 | 6,854 | 2,917 |
| **Asilimia ya watahiniwa** | 32.27 | 21.48 | 13.11 | 23.06 | 8.95 | 0.79 | 0.34 |

Swali lililenga kupima uwezo wa mtahiniwa katika matumizi ya msamiati wa Kiswahili sanifu. Asilimia 21.48 ya watahiniwa walichagua jibu B "Rahani" ambalo ndilo jibu sahihi. Watahiniwa 279,172 sawa na asilimia 32.27 walichagua kipotoshi A "Posho" ambacho si jibu sahihi na huenda walifanya hivyo kwa sababu walifananisha neno "posho" na "poni" kwa kuwa yote yanaanza na -po-. Hii inaonesha wazi kuwa watahiniwa husika hawakuwa na ujuzi wa msamiati huo kwani hata uchaguzi wa vipotoshi C "Mali", D "Mkopo" na E "Pesa" unadhihirisha watahiniwa kutokuwa na ujuzi wa msamiati kwani maneno hayo hutumika mara kwa mara katika miktadha mbalimbali lakini hawakuweza kuyatofautisha na neno "poni". Aidha watahiniwa 6,854 hawakujibu kabisa swali hilo wakati watahiniwa 2,917 walichagua jibu zaidi ya moja ikionesha kuwa hawakuwa na ujuzi stahiki.

**Swali la 15**: Shuleni kwetu kuna upungufu wa ________. Ni neno lipi hukamilisha tungo hiyo kwa usahihi?

A. Thamani
B. Thamini
C. Dhamini
D. Zamani
E. Samani

Majibu ya watahiniwa

| Chaguo | A | B | C | D | E* | Wasiojibu | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya watahiniwa** | 302,336 | 53,346 | 73,481 | 77,917 | 351,092 | 3,603 | 3,331 |
| **Asilimia ya watahiniwa** | 34.95 | 6.17 | 8.49 | 9.0 | 40.58 | 0.42 | 0.39 |

Swali lililenga kupima uwezo wa mtahiniwa katika utumizi wa lugha. Watahiniwa 351,092 sawa na asilimia 40.58 walichagua E "Samani" ambalo ndilo jibu sahihi. Watahiniwa wengi pia (302,336) walichagua kipotoshi A "Thamani" ambalo sio jibu sahihi jambo linaloonesha kuwa walikosa maarifa ya kisemantikia ya Kiswahili. Watahiniwa hao walivutiwa na neno "Thamani"

kwa kuwa matamshi yake yanataka kufanana na “Samani” ingawa maneno hayo yana maana tofauti. Athari ya kimatamshi zinaweza pia kuwa zilichangia kwa watahiniwa waliochagua kipotoshi D “zamani” badala ya “samani”.

**Swali la16**: “Mtoto ametengeneza toroli ya mti” Wingi wa sentensi hii ni upi?

A. Watoto wametengeneza toroli za miti
B. Watoto wametengeneza matoroli ya mti
C. Watoto ametengeneza matoroli ya miti
D. Watoto wametengeneza toroli za mti
E. Watoto wametengeneza matoroli ya miti

Majibu ya watahiniwa

| Chaguo | A* | B | C | D | E | Wasiojibu | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Idadi ya watahiniwa | 158,683 | 135,610 | 120,324 | 59,697 | 384,612 | 3,122 | 3,058 |
| Asilimia ya watahiniwa | 18.34 | 15.68 | 13. 91 | 6.9 | 44.46 | 0.36 | 0.35 |

Swali lililenga katika kupima ujuzi wa mtahiniwa katika mada ya upatanisho wa kisarufi. Asilimia 18.34 walichagua jibu A “Watoto wametengeneza toroli za miti” ambalo ndilo jibu sahihi. Watahiniwa 384,612 ambao ni sawa na asilimia 44.46 walichagua kipotoshi E “Watoto wametengeneza matoroli ya miti” hali inayoonesha kuwa walikosa maarifa ya dhana ya umoja na wingi hasa kuhusu neno “toroli” ambalo ni nomino isiyokuwa na umoja na wingi katika upatanisho wa kisarufi. Uchaguzi wa vipotoshi B, C na D unaonesha kuwa watahiniwa walishindwa kuiweka dhana ya wingi pale ilipohitajika kwa mfano <u>ma</u>toroli badala ya toroli, <u>a</u>metengeneza badala ya <u>wa</u>metengeneza na <u>m</u>ti badala ya <u>m</u>iti hivyo kushindwa kupata upatanisho wa kisarufi ulio sahihi.

**Swali la 17:** “Muda mfupi atakuwa anaingia uwanjani.” Sentensi hii ipo katika wakati gani?

A. Uliopo
B. Uliopita
C. Wa mazoea
D. Ujao
E. Timilifu

Majibu ya watahiniwa

| Chaguo | A | B | C | D* | E | Wasiojibu | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Idadi ya watahiniwa | 194,364 | 69,510 | 86,871 | 417,631 | 92,272 | 2,140 | 2,318 |
| Asilimia ya watahiniwa | 22.47 | 8.03 | 10.04 | 48.28 | 10.67 | 0.25 | 0.27 |

Swali lililenga katika kupima ujuzi wa mtahiniwa katika matumizi ya njeo ya wakati. Asilimia 48.28 ya watahiniwa walichagua D “Ujao” ambalo ndilo jibu sahihi. Asilimia 22.47 walichagua kipotoshi A “Uliopo” ambacho sio jibu sahihi. Watahiniwa hao walikosa uelewa wa maumbo mbalimbali yanayowakilisha dhana ya njeo katika Sarufi ya Kiswahili. Aidha uchaguzi wa vipotoshi B, C na E unaonesha kuwa watahiniwa hao walishindwa kuelewa kuwa kitenzi kisaidizi ambacho hutangulia kitenzi kikuu, huonesha njeo ya wakati. Mfano kitenzi kisaidizi “atakuwa” kina kiambishi **-ta-** ambacho ni kiambishi cha njeo ya wakati ujao hivyo kuonesha kuwa tendo hilo linatarajiwa kutendeka.

**Swali la 18**: “Ni neno lipi kati ya haya yafuatayo halilandani na mengine?

A. Fikiri
B. Dodosa
C. Uliza
D. Hoji
E. Saili.

Majibu ya Watahiniwa

| Chaguo | A* | B | C | D | E | Wasiojibu | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Idadi ya watahiniwa | 161,786 | 268,671 | 63,156 | 45,207 | 321,688 | 2,229 | 2,369 |
| Asilimia ya watahiniwa | 18.7 | 31.06 | 7.3 | 5.23 | 37.18 | 0.26 | 0.27 |

Swali lililenga kupima uelewa wa mtahiniwa katika matumizi ya msamiati. Asilimia 18.7 walichagua jibu A “Fikiri” ambalo ndilo jibu sahihi. Watahiniwa 321,688 ambao ni sawa na asilimia 37.18 walichagua kipotoshi E “Saili” ambacho sio jibu sahihi. Watahiniwa hao walishindwa kuhusisha kipotoshi E na vipotoshi B, C, D kwamba yote ni maneno yenye mfanano wa kimaana katika kipengele cha kutaka kupata taarifa ijapokuwa katika mipangilio tofauti.

**Swali la 19:** Juma aliondoka hivi punde. Maneno “hivi punde” yana maana ipi?

A. Haraka
B. Muda mrefu
C. Karibuni
D. Kwa pupa
E. Kwa haraka.

Majibu ya watahiniwa

| Chaguo | A | B | C* | D | E | Wasiojibu | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Idadi ya watahiniwa | 103,641 | 155,320 | 458,835 | 53,079 | 89,314 | 2,589 | 2,328 |
| Asilimia ya watahiniwa | 11.98 | 17.95 | 53.04 | 6.14 | 10.32 | 0.3 | 0.27 |

Swali lililenga kupima uwezo wa mtahiniwa katika kutumia aina ya maneno na hasa vielezi. Asilimia 53.04 ya watahiniwa waliofanya mtihani wa Kiswahili walichagua jibu C “Karibuni” ambalo ndilo jibu sahihi. Watahiniwa 155,320 sawa na asilimia 17.95 walichagua kipotoshi B “Muda Mrefu”. Watahiniwa hao walichanganya njeo ya wakati iliyotumika katika kitenzi “aliondoka” bila ya kuzingatia kuwa matakwa ya swali yalijikita katika maneno “hivi punde” ambayo maana yake ni “karibuni.” Asilimia 11.98 ya watahiniwa walichagua kipotoshi A “Haraka” na asilimia 10.32 walichagua E “Kwa haraka” hali inayoonesha kuwa walishindwa kutofautisha maana ya maneno hayo na maneno “hivi punde”.

**Swali la 20:** Neno lipi ni kisawe cha neno adili?

A. Ujinga
B. Wema
C. Uovu
D. Ujasiri
E. Ukatili.

Majibu ya watahiniwa

| Chaguo | A | B* | C | D | E | Wasiojibu | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Idadi ya watahiniwa | 80,447 | 414,361 | 141,218 | 120,519 | 100,869 | 4,585 | 3,107 |
| Asilimia ya watahiniwa | 9.3 | 47.9 | 16.32 | 13.93 | 11.66 | 0.53 | 0.36 |

Swali lililenga kupima uelewa wa mtahiniwa kuhusu visawe vya maneno. Asilimia 47.9 ya watahiniwa walichagua jibu B “Wema” ambalo ndilo jibu

sahihi. Watahiniwa 141,218 walichagua kipotoshi C “Uovu” ambalo ni kinyume cha neno “Wema” hali inayoashiria kuwa ama hawakuelewa matakwa ya swali au hawakuwa na uelewa unaotakiwa wa visawe sahihi vya maneno. Uchaguzi wa vipotoshi A, D na E ulidhihirisha pia kuwa baadhi ya watahiniwa hawakuwa na ujuzi wa visawe sahihi vya maneno. Aidha watahiniwa hao walishindwa kuelewa maana ya neno ‘adili’ ili kuweza kupata kisawe sahihi.

## 2.2 Sehemu B: Lugha ya Kifasihi

**Swali la 21**: “Mwanzo wa ngoma ni lele.” Methali inayofanana na hii kati ya hizi zifuatazo ni ipi?

A. Dawa ya moto ni moto
B. Dalili ya mvua ni mawingu
C. Dira ya binadamu ni kichwa
D. Dawa ya jipu ni kulipasua
E. Mtoto wa nyoka ni nyoka.

Majibu ya watahiniwa

| **Chaguo** | **A** | **B*** | **C** | **D** | **E** | **Wasiojibu** | **Mengine** |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya watahiniwa** | 119,725 | 415,204 | 130,123 | 71,603 | 121,373 | 3,914 | 3,164 |
| **Asilimia ya watahiniwa** | 13.84 | 47.99 | 15.04 | 8.28 | 14.03 | 0.45 | 0.37 |

Swali lililenga kupima uelewa wa mtahiniwa kuhusu tanzu za semi na hasa methali. Asilimia 47.99 ya watahiniwa walichagua jibu B “Dalili ya Mvua ni Mawingu” ambalo ndilo jibu sahihi. Asilimia 15.04 ya watahiniwa waliochagua kipotoshi C “Dira ya binadamu ni Kichwa” walishindwa kuelewa kuwa neno “dira” ni njia na kamwe haiwezi kuwa na maana sawa na “Mwanzo wa ngoma ni lele” ambayo huendana na “Dalili za mvua ni mawingu”. Methali hizo huashiria jambo fulani hutokea baada ya jambo lingine kutokea.

**Swali la 22:** **“**Akutendaye mtende usimche akutendaye.” Methali hii inatoa funzo gani?

A. Mwovu akomeshwe kwa adhabu kali
B. Akufanyiae maovu usimche
C. Mwovu akwepwe kwa kutenda
D. Anayekutendea usilipize kisasi
E. Mwovu akwepwe kwa kutendwa.

Majibu ya watahiniwa

| Chaguo | A* | B | C | D | E | Wasiojibu | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Idadi ya watahiniwa | 153,611 | 231,674 | 70,615 | 349,905 | 52,102 | 4,273 | 2,926 |
| Asilimia ya watahiniwa | 17.76 | 26.78 | 8.16 | 40.45 | 6.02 | 0.49 | 0.34 |

Swali lililenga kupima uelewa wa mtahiniwa kuhusu methali na mafunzo yatokanayo na methali hizo. Ni asilimia 17.76 tu ya watahiniwa waliofanya mtihani wa Kiswahili ndio waliochagua A "mwovu akomeshwe kwa adhabu kali" ambalo ndilo jibu sahihi. Watahiniwa 349,905 sawa na asilimia 40.45 walichagua kipotoshi D "Anayekutendea usilipize kisasi" ambalo sio jibu sahihi. Inawezekana watahiniwa hao walichagua jibu hilo kwa kuhusianisha swali na dhana ya imani isemayo "Akupigaye shavu la kushoto mgeuzie na la kulia." Aidha watahiniwa wengine walichanganya methali hiyo na ile isemayo, "Akunyang'anyaye kanzu yako mwachie na joho lako." Hivyo walishindwa kuelewa kuwa methali waliyoulizwa ilikuwa inaelekeza kuwa akutendaye mabaya/maovu nawe umkomeshe ili asidiriki kukutendea tena ubaya na kamwe sio wa kumkwepa au kumwacha.

**Swali la 23:** "Uzuri wa mkakasi ndani _______________." Ni kifungu kipi kati ya vifuatavyo kinakamilisha methali hiyo?

A. kuna mti laini
B. kipande cha mdalasini
C. kipande cha mti
D. ni mti mkavu
E. kipande laini.

Majibu ya watahiniwa

| Chaguo | A | B | C* | D | E | Wasiojibu | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Idadi ya watahiniwa | 204,529 | 190,389 | 235,460 | 138,316 | 88,881 | 4,630 | 2,901 |
| Asilimia ya watahiniwa | 23.64 | 22.01 | 27.22 | 15.99 | 10.27 | 0.54 | 0.34 |

Swali lililenga kupima uelewa wa mtahiniwa kuhusu ukamilishaji wa methali aliyopewa. Asilimia 27.22 ya watahiniwa walichagua C "Kipande cha mti" ambalo ndilo jibu sahihi. Watahiniwa 204,529 sawa na asilimia 23.64 waliochagua A "kuna mti laini" walikuwa na uelewa kidogo wa methali hiyo na walitambua kuwa neno mti ni miongoni mwa maneno yaliyopo katika ukamilishaji wa methali hiyo. Hata hivyo hawakuwa na uelewa sahihi na hivyo kuchagua jibu lisilo sahihi kwa kuvutiwa na kuwepo kwa neno "mti" katika kipotoshi hicho.

Aidha, watahiniwa 190,389 sawa na asilimia 22.01 walichagua B “kipande cha mdalasini” ambao nao wanaonekana kuvutiwa na uwepo wa neno kipande bila kusoma kwa umakini ni kipande cha nini. Uchaguzi wa vipotoshi D na E unadhihirisha kuwa watahiniwa hawakuwa na uelewa wa matakwa ya swali. Swali hilo lilitarajiwa kuwa miongoni mwa maswali ambayo watahiniwa wangeweza kuyajibu kwa usahihi kwa kuwa methali hiyo hutumika mara kwa mara katika jamii.

**Swali la 24:** Msemo upi kati ya ifuatayo unakamilisha sentensi, “Kinjekitile alijaribu_______________ lakini baadaye hakuitekeleza.”

A. kuweka hadhari
B. kuweka nadhiri
C. kuweka hadhira
D. kuweka nadharia
E. kuweka nadhari.

Majibu ya watahiniwa

| Chaguo | A | B* | C | D | E | Wasiojibu | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Idadi ya watahiniwa | 181,854 | 295,113 | 149,458 | 169,380 | 62,506 | 3,842 | 2,953 |
| Asilimia ya watahiniwa | 21.02 | 34.11 | 17.28 | 19.58 | 7.23 | 0.44 | 0.34 |

Swali lililenga katika kupima uelewa wa mtahiniwa kuhusu matumizi ya misemo mbalimbali ya Kiswahili. Asilimia 34.11 ya watahiniwa walichagua jibu B “kuweka nadhiri” ambalo ndilo jibu sahihi. Uchaguzi wa vipotoshi A na D kwa asilimia 21.02 na asilimia 19.58 unadhihirisha kuwa watahiniwa hao walishindwa kuelewa maana ya neno “hadhari” ambalo linamaanisha tahadhari na neno “nadharia” ambalo linamaanisha maelezo au mawazo. Jumla ya watahiniwa 149,458 walichagua kipotoshi C “hadhira” ambacho kinamaanisha wasikilizaji. Hivyo uchambuzi unaonesha kuwa watahiniwa hawakuweza kutambua kuwa maneno yote hayo yaliyowekwa kwenye vipotoshi yana maana tofauti kabisa na neno “nadhiri” ambalo maana yake ni ahadi.

**Swali la 25:** Tegua kitendawili kisemacho, “Atembeapo kila mara huringa hata kama kuna adui.”

A. Bata
B. Konokono
C. Kobe
D. Kanga
E. Kinyonga

Majibu ya Watahiniwa

| Chaguo | A | B | C | D | E* | Wasiojibu | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya watahiniwa** | 55,771 | 75,860 | 52,113 | 30,576 | 643,290 | 2,344 | 5,152 |
| **Asilimia ya watahiniwa** | 6.45 | 8.77 | 6.02 | 3.53 | 74.36 | 0.27 | 0.6 |

Swali lililenga kupima uelewa wa mtahiniwa kuhusu semi na hasa vitendawili. Asilimia 74.36 ya watahiniwa walichagua E "Kinyonga" ambalo ndilo jibu sahihi. Swali la 25 ni mojawapo ya maswali yaliyojibiwa vizuri na watahiniwa wengi kwa sababu linaonesha kuwa walikuwa na uelewa wa kitendawili hicho ambacho hutumika mara kwa mara. Asilimia 24.77 ya watahiniwa walichagua kati ya vipotoshi A, B, C na D hali inayoonesha kuwa watahiniwa husika hawakuwa na uelewa wa kutosha kuhusu vitendawili na hususan kitendawili walichoulizwa katika swali hili.

**Swali la 26:** "Siku hizi siri za mafisadi zimeanikwa juani". Usemi "kuanikwa juani" una maana ipi kati ya hizi zifuatazo?

A. Kuelezwa waziwazi
B. Kusemwa hadharani
C. Kusemwa nje ya kikao
D. Kuelezwa hadharani
E. Kusemwa jukwaani

Majibu ya watahiniwa

| Chaguo | A | B | C | D* | E | Wasiojibu | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya watahiniwa** | 23,5476 | 373,578 | 76,118 | 131,281 | 42,531 | 3,155 | 2,967 |
| **Asilimia ya watahiniwa** | 27.22 | 43.18 | 8.8 | 15.18 | 4.92 | 0.36 | 0.34 |

Swali lililenga kupima uwezo wa watahiniwa kuhusu matumizi ya semi katika lugha ya Kiswahili. Asilimia 15.18 ya watahiniwa walichagua jibu D ambalo lilikuwa linaelezea usemi "kuanikwa juani" kuwa ni sawa na "kuelezwa hadharani". Jibu hilo lilikuwa ni jibu sahihi kwa sababu kuelezwa hadharani ni kutoa maelezo au ufafanuzi kuhusu jambo fulani katika mkusanyiko wa watu wengi. Hivyo, "kuanikwa juani" inamaanisha kuelezwa hadharani.

Watahiniwa 373,578 sawa na asilimia 43.18 walichagua kipotoshi B "Kusemwa hadharani" kunakomaanisha kutamka bila kutoa ufafanuzi ambalo sio jibu sahihi. Watahiniwa waliochagua vipotoshi A, C na E ambayo

yalikuwa si majibu sahihi, walishindwa kutofautisha kati ya kuelezwa kwa jambo hadharani na kuelezwa waziwazi. Kuelezwa waziwazi kunaweza kuwa mbele ya watu au hata ndani ya nyumba. Kusemwa nje ya kikao kwaweza kuhusisha au kutohusisha hadhira. Kusemwa jukwaani kunaweza kufanyika bila hadhira au hadhira kutokuhusishwa. Hivyo uchaguzi wa vipotoshi A, B, C na E unaonesha kuwa watahiniwa hawakuwa na uelewa wa kutosha kuhusu tofauti hizo.

**Swali la 27**: Methali ipi kati ya zifuatazo ina maana sawa na hii isemayo “Meno ya mbwa hayaumani”

A. Mwana kidonda, mjukuu kovu
B. Akipenda chongo, huita kengeza
C. Damu nzito, kuliko maji
D. Heri mrama, kuliko kuzama
E. Maneno matupu, hayavunji mfupa

Majibu ya watahiniwa

| Chaguo | A | B | C* | D | E | Wasiojibu | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Idadi ya watahiniwa | 115,540 | 93,116 | 316,864 | 67,947 | 263,675 | 4,399 | 3,565 |
| Asilimia ya watahiniwa | 13.36 | 10.76 | 36.63 | 7.85 | 30.48 | 0.51 | 0.41 |

Swali lilikuwa linapima uwezo wa watahiniwa kutambua methali iliyo sawa na “Meno ya mbwa hayaumani”. Asilimia 36.63 ya watahiniwa walijibu swali kwa usahihi kwa kuchagua jibu C “Damu nzito kuliko maji”. Watahiniwa 263,675 sawa na asilimia 30.48 walichagua kipotoshi E “Maneno matupu, hayavunji mfupa” ambayo inamaanisha kusema bila kutenda hakuwezi kukamilisha jambo tofauti na maana ya methali waliyopewa.

Waliochagua vipotoshi A, B na D ambavyo si majibu sahihi ya swali, walishindwa kuifananisha methali waliyopewa na maana yake kuwa wenye kuhusiana hawawezi kutendeana ubaya. Watahiniwa waliochagua vipotoshi hivi kwa ujumla walikuwa ni asilimia 31.97 ambao walikosa ujuzi wa kuchambua vitu vinavyofanana na vile visivyofanana.

**Swali la 28**: “Tatizo la ufisadi limeota mizizi katika nchi yetu”. Usemi “kuota mizizi” una maana ipi?

A. Kuibuka
B. Kuchipuka
C. Kushamiri
D. Kuongezeka
E. Kuenea

Majibu ya watahiniwa

| Chaguo | A | B | C* | D | E | Wasiojibu | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Idadi ya watahiniwa | 111,367 | 130,042 | 233,964 | 198,307 | 183,549 | 4,444 | 3,433 |
| Asilimia ya watahiniwa | 12.87 | 15.03 | 27.04 | 22.92 | 21.22 | 0.51 | 0.4 |

Swali hili lilikuwa linapima ufahamu wa matumizi ya semi mbalimbali za Kiswahili ambapo asilimia 27.04 ya watahiniwa ndio waliojibu swali kwa usahihi kwa kuchagua jibu C lililoonesha kuwa semi 'kuota mizizi" ni sawa na "kushamiri" ikiwa na maana ya kuongezeka kwa jambo kwa kasi kubwa. Watahiniwa 198,307 sawa na asilimia 22.92 walichagua kipotoshi D "kuongezeka". Neno kuongezeka liliwavutia watahiniwa hao lakini walisahau kuwa maneno "kuota mizizi" yanaonesha msisitizo kuwa jambo hilo linajitokeza kwa kasi kubwa wakati neno "kuongezeka" halioneshi ukubwa wa ongezeko kwani linaweza kutumika hata kwa ongezeko dogo la jambo fulani.

Asilimia 12.87 ya watahiniwa waliochagua kipotoshi A "Kuibuka" walishindwa kuelewa maana ya neno hilo ambayo ni kutokea kwa jambo bila kutarajiwa. Aidha asilimia 15.03 ya watahiniwa waliochagua kipotoshi B hawakuelewa kuwa maana ya neno "kuchipuka" ni kuonekana juu ya ardhi. Uteuzi wa vipotoshi D na E unaonesha kwamba watahiniwa husika walikosa ujuzi wa kutambua maana sahihi ya usemi huo kwa kushindwa kuvitofautisha vipotoshi hivyo na maana ya nahau kama utanzu wa semi za Kiswahili.

**Swali la 29**: Tegua kitendawili kifuatacho "Kondoo wangu kachafua njia nzima."

A. Konokono
B. Jongoo
C. Tandu
D. Mjusi
E. Kinyonga

Majibu ya watahiniwa

| Chaguo | A* | B | C | D | E | Wasiojibu | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Idadi ya watahiniwa | 436,347 | 178,268 | 136,418 | 54,613 | 52,124 | 4,317 | 3,019 |
| Asilimia ya watahiniwa | 50.44 | 20.61 | 15.77 | 6.31 | 6.03 | 0.5 | 0.35 |

Swali lilikuwa linapima uwezo wa watahiniwa kuunda dhana inayowiana na kitendawili hicho kwa kuhusianisha na mazingira ya semi husika. Watahiniwa 436,347 sawa na asilimia 50.44 waliweza kuchagua jibu sahihi ambalo ni

A “Konokono”. Asilimia 20.61 walichagua B “Jongoo” na asilimia 15.77 walichagua C “Tandu” ambao wote ni wadudu wanaotambaa na huweza kuacha alama wanapopita lakini ni tofauti na konokono ambaye huacha utandu kila anakopita. Hivyo watahiniwa hao pamoja na wale waliochagua vipotoshi D na E walishindwa kuunda dhana ya swali iliyowataka kutambua tofauti ya wadudu wanaotambaa na wale wanaoacha utando kila wanakopita.

**Swali la 30**: “Ntandu alikuwa na kichwa cha panzi”. Msemo “kichwa cha panzi” una maana ipi?

A. Msikivu sana
B. Msahaulifu sana
C. Ana utambuzi
D. Ana kumbukumbu
E. Mtiifu sana

Majibu ya watahiniwa

| Chaguo | A | B* | C | D | E | Wasiojibu | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Idadi ya watahiniwa | 137,194 | 361,545 | 103,476 | 178,063 | 76,464 | 4,978 | 3,386 |
| Asilimia ya watahiniwa | 15.86 | 41.79 | 11.96 | 20.58 | 8.84 | 0.58 | 0.39 |

Swali lilikuwa linapima uwezo wa mtahiniwa wa kuchambua misemo mbalimbali na matumizi yake katika mazingira au muktadha. Asilimia 41.79 ya watahiniwa walijibu swali kwa usahihi kwa kuonesha maana halisi ya msemo “kichwa cha panzi” ambayo ni chaguzi B “msahaulifu sana”. Asilimia 20.58 walichagua kipotoshi D “Ana kumbukumbu” jibu ambalo halikuwa sahihi na lilikuwa ni kinyume na jibu sahihi “msahaulifu sana”. Waliochagua vipotoshi A na C walishindwa kufafanua maana ya msemo huo kutokana na vipotoshi hivyo vyote kuhusisha milango ya fahamu. Aidha watahiniwa waliochagua kipotoshi E hawakuwa na uelewa wa nahau hiyo. Kilichohitajika ili kuweza kujibu swali kwa usahihi ni uelewa wa nahau hiyo.

## 2.3 Sehemu C: Ufahamu

Katika sehemu hii watahiniwa walitakiwa kusoma kifungu cha habari na kujibu maswali yaliyotokana na kifungu hicho. Kifungu walichopewa kilisomeka kama ifuatavyo:

*Uuzaji wa mazao ni tendo la kubadilisha mazao kwa fedha. Mkulima anampa mtu mwingine mazao yake ili yeye apewe fedha. Uuzaji huu unaweza kufanywa na mkulima mwenyewe au dalali. Kituo kikubwa*

*cha kuuzia mazao haya ni soko au gulio. Serikali huwa inawashauri wakulima kuanzisha vyama vya ushirika. Vyama hivi vitakuwa na kazi ya kununua mazao ya wakulima na kuyauza ndani na nje ya nchi. Tatizo kubwa la vyama vya ushirika ni ile tabia ya kukopa mazao kwa wakulima halafu kuyauza ndipo ipatikane fedha ya kuwalipa wakulima. Mfumo huu unatakiwa uwe unaratibiwa vizuri na wakulima, kwani mali bila daftari hupotea bila habari.*

*Siku hizi kuna soko huria. Watu binafsi hujitokeza kununua mazao kwa bei nzuri na hulipa fedha kwa wakati huo huo. Kwa njia hii huwasaidia wakulima kupata soko la mazao yao. Hata hivyo, wakulima wanapaswa kuwa makini kwa kuwa wanunuzi wengine ni matapeli. Mashambega hawa hufanya hila kwa kutumia mizani zisizo sahihi na hivyo wakulima huambulia fedha kichele tu. Hali hii huwaletea simanzi wakulima, lakini pamoja na masononeko hayo, kwa kuwa walanguzi hutoa pesa papo kwa papo, wakulima wengi huona bora kuwauzia walanguzi kuliko kuikopesha serikali. Wahenga walisema heri kenda kuliko kumi nenda uje.*

**Swali la 31**: Kichwa cha habari kinachofaa kwa habari uliyosoma ni kipi?

A. Soko la mazao
B. Mazao na walanguzi
C. Biashara isiyolipa
D. Biashara ya mazao
E. Kubadilisha mazao

Majibu ya watahiniwa

| Chaguo | A | B | C | D* | E | Wasiojibu | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya watahiniwa** | 262,657 | 94,100 | 87,063 | 235,600 | 177,317 | 4,545 | 3,824 |
| **Asilimia ya watahiniwa** | 30.36 | 10.88 | 10.06 | 27.23 | 20.5 | 0.53 | 0.44 |

Swali lilikuwa linapima ufahamu wa mtahiniwa baada ya kusoma kifungu cha habari. Asilimia 27.23 ya watahiniwa waliweza kujibu swali kwa usahihi kwa kuchagua kichwa cha habari ambacho ni D “Biashara ya mazao” kutokana na usomaji wa makini, uelewa na uwezo wa kuyatambua mawazo makuu katika habari waliyosoma. Asilimia 30.36 walichagua kipotoshi A kwavile hawakuwa na uelewa kuwa soko la mazao linahusisha mkusanyiko wa wauzaji wengi wanaouza bidhaa rejareja. Hivyo walishindwa kuelewa kuwa kifungu hicho cha habari kilihusisha biashara ya mazao ya jumla pamoja na soko huria. Uchaguzi wa vipotoshi B, C na E ulifanywa na watahiniwa ambao walishindwa kutambua kuwa vipotoshi hivyo havitoi muhtasari wa mawazo makuu ya habari waliyopewa.

**Swali la 32**: Neno "simanzi" kama lilivyotumika katika habari hii lina maana **tofauti** na lipi?

A. Masononeko
B. Mawazo
C. Majonzi
D. Masikitiko
E. Huzuni

Majibu ya watahiniwa

| Chaguo | A | B* | C | D | E | Wasiojibu | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Idadi ya watahiniwa | 272,234 | 191,909 | 144,698 | 126,328 | 121,919 | 4,539 | 3,479 |
| Asilimia ya watahiniwa | 31.47 | 22.18 | 16.73 | 14.6 | 14.09 | 0.52 | 0.4 |

Swali hili lilikuwa linapima ufahamu wa kusoma na kuelewa maana ya maneno yaliyotumika katika habari. Asilimia 22.18 ya watahiniwa walijibu swali kwa usahihi kwani waliweza kutofautisha neno "simanzi" na "mawazo" kama lilivyotumika katika habari. Asilimia 31.47 walichagua kipotoshi A kwa kuwa walikosa ujuzi wa kutambua neno "Masononeko" lilivyotumika katika kifungu cha habari maana yake ni sawasawa na neno "simanzi". Hivyo watahiniwa walitafsiri matakwa ya swali tofauti na jinsi ilivyotakiwa. Aidha uchaguzi wa vipotoshi C, D na E unaonesha kuwa watahiniwa hawakuelewa matakwa ya swali kwani badala ya kutaja neno lenye maana tofauti na "simanzi" walionesha kisawe cha neno hilo.

**Swali la 33**: Vyama vya ushirika vinahitaji kuwa na nini?

A. Pesa taslimu
B. Utaratibu mzuri
C. Utunzaji kumbukumbu
D. Kuondoa matapeli
E. Udhibiti mzuri

Majibu ya watahiniwa

| Chaguo | A | B* | C | D | E | Wasiojibu | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Idadi ya watahiniwa | 236,176 | 268,711 | 165,355 | 129,310 | 58,050 | 4,779 | 2,725 |
| Asilimia ya watahiniwa | 27.3 | 31.06 | 19.11 | 14.95 | 6.71 | 0.55 | 0.31 |

Swali lilikuwa linapima ufahamu wa kusoma kwa makini kifungu cha habari. Ni asilimia 31.06 pekee ya watahiniwa ndio walioweza kujibu swali kwa usahihi kwa kuchagua jibu B “Utaratibu mzuri” kwasababu aya ya kwanza ilikuwa inajitosheleza kueleza jambo lililotakiwa katika uimarishaji wa vyama vya ushirika. Watahiniwa waliochagua vipotoshi A, C, D na E walikosa ujuzi wa kusoma kwa makini na kupata ufahamu kutoka katika kifungu walichopewa. Aidha watahiniwa waliochagua kipotoshi A ambao ni asilimia 27.3 walichanganywa na neno ‘pesa’ kwani walifikiri vyama vya ushirika huhitaji fedha ili kuviendesha na kuviimarisha.

**Swali la 34:** “Fedha kichele”. Nahau hii ina maana ipi?

A. Fedha kidogo
B. Fedha kiasi
C. Fedha ndogondogo
D. Fedha taslimu
E. Fedha waziwazi

Majibu ya watahiniwa

| Chaguo | A* | B | C | D | E | Wasiojibu | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya watahiniwa** | 502,594 | 82,530 | 138,636 | 83,108 | 53,189 | 2,758 | 2,291 |
| **Asilimia ya watahiniwa** | 58.1 | 9.54 | 16.03 | 9.61 | 6.15 | 0.32 | 0.26 |

Swali lilikuwa linapima maarifa ya mtahiniwa kuhusu semi za Kiswahili. Asilimia 58.1 walijibu swali kwa usahihi kwa kuchagua jibu A “Fedha kidogo” kwa kuwa na maarifa na utanzu wa semi hasa nahau. Aidha, ni semi ambayo imezoeleka katika jamii. Watahiniwa waliochagua vipotoshi B, C na D walikosa maarifa kuhusu maana zinazowakilishwa na semi za Kiswahili hasa nahau. Aidha watahiniwa walipotoshwa na maneno “kidogo”, “kiasi”, “ndogondogo” na “taslimu” ambayo yalikuwa na mfanano kwa kuwa yote yanaelezea kuhusu kiasi cha fedha.

**Swali la 35**: Kisawe cha neno tapeli ni kipi?

A. Mlanguzi
B. Mhujumu
C. Fisadi
D. Mlaghai
E. Mnyonyaji

Majibu ya watahiniwa

| Chaguo | A | B | C | D* | E | Wasiojibu | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya watahiniwa** | 152,932 | 81,277 | 273,938 | 198,371 | 154,558 | 1,669 | 2,361 |
| **Asilimia ya watahiniwa** | 17.68 | 9.4 | 31.67 | 22.93 | 17.87 | 0.19 | 0.27 |

Swali lilikuwa linapima maarifa ya mtahiniwa kuhusu maana ya misamiati ya Kiswahili sanifu. Asilimia 22.93 ya watahiniwa walijibu swali kwa usahihi kutokana na maarifa waliyokuwa nayo na hivyo walichagua D “Mlaghai” ambalo ndilo maana sahihi ya neno ‘tapeli’. Jumla ya watahiniwa 273,938 sawa na asilimia 31.67 walichagua C “Fisadi” ambalo si jibu sahihi. Watahiniwa hao walivutika na kipotoshi hicho kwa kuwa ufisadi unahusisha kujipatia mali kwa njia zisizo sahihi hivyo watahiniwa walishindwa kutofautisha neno hilo na neno “tapeli”. Aidha, neno “Fisadi” linaweza pia kuwa liliwavutia zaidi watahiniwa kwa kuwa ni neno lililo na mashiko katika jamii zetu ambalo hivi sasa linalotumika sana. Watahiniwa waliochagua vipotoshi A “Mlanguzi” na E “Mnyonyaji”, walikosa maarifa ya kuwawezesha kufahamu maana za misamiati na hasa ikizingatiwa kuwa maneno hayo yanahusiana ingawa yana maana tofauti.

**Swali la 36**: Methali “Heri kenda shika kuliko kumi nenda uje,” inatoa funzo gani?

A. Tuone umuhimu wa kuwa nacho
B. Kidogo tulichonacho kitatufaa zaidi
C. Kuthamini kidogo tunachopata
D. Turidhike na chetu si cha jirani
E. Kuthamini mali tuliyonayo.

Majibu ya watahiniwa

| Chaguo | A | B | C* | D | E | Wasiojibu | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya watahiniwa** | 91,487 | 243,717 | 201,491 | 226,924 | 94,876 | 4,243 | 2,368 |
| **Asilimia ya watahiniwa** | 10.58 | 28.17 | 23.29 | 26.23 | 10.97 | 0.49 | 0.27 |

Swali lilikuwa linapima matumizi ya semi za Kiswahili. Asilimia 23.29 walijibu swali kwa kuchagua jibu C “Kuthamini kidogo tunachopata” ambalo ni jibu sahihi. Watahiniwa hao walikuwa wanajua matumizi sahihi ya methali hiyo. Watahiniwa waliochagua vipotoshi A, B, D na E walikosa maarifa kuhusu maana inayowakilishwa na semi za Kiswahili hasa methali.

**Swali la 37**: Katika habari uliyoisoma jamii inaaswa kuhusu nini?

A. Umuhimu wa kuorodhesha mali
B. Umuhimu wa kumbukumbu katika biashara
C. Umuhimu wa kutunza biashara ndani ya daftari
D. Umuhimu wa biashara kuorodheshwa wazi
E. Umuhimu kwa mfanyabiashara kuwa na daftari.

Majibu ya watahiniwa

| Chaguo | A | B* | C | D | E | Wasiojibu | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Idadi ya watahiniwa | 106,475 | 284,981 | 178,175 | 73,495 | 212,943 | 5,948 | 3,089 |
| Asilimia ya watahiniwa | 12.31 | 32.94 | 20.6 | 8.5 | 24.61 | 0.69 | 0.36 |

Swali lilikuwa linapima tathmini ya uelewa wa watahiniwa kuhusu habari. Asilimia 32.94 walijibu swali kwa kuchagua jibu B “umuhimu wa kumbukumbu katika biashara” ambalo ni sahihi. Watahiniwa hao waliweza kuisoma habari na kuelewa dhima yake kwa jamii. Watahiniwa waliochagua vipotoshi A, C, D na E walipotoshwa na dhana ya ‘umuhimu’ iliyotumika katika kila kipotoshi.

**Swali la 38**: Neno lipi kati ya yafuatayo ni kinyume cha neno “hila”?

A. Udanganyifu
B. Ughilibu
C. Uungwana
D. Ujanja
E. Unadhifu.

Majibu ya watahiniwa

| Chaguo | A | B | C* | D | E | Wasiojibu | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Idadi ya watahiniwa | 273,208 | 110,956 | 241,424 | 133,381 | 97,639 | 5,209 | 3,289 |
| Asilimia ya watahiniwa | 31.58 | 12.83 | 27.91 | 15.42 | 11.29 | 0.6 | 0.38 |

Swali lilikuwa linapima uwezo wa mtahiniwa wa kuunda dhana iliyo kinyume na neno “hila”. Asilimia 27.91 walijibu swali kwa usahihi kwa kuchagua jibu C. Watahiniwa husika waliweza kuunda dhana iliyo kinyume na neno “hila” ambalo ni “uungwana”. Neno “uungwana” lilikuwa na tofauti kubwa ya kimaana ukilinganisha na vipotoshi vingine vya swali hilo. Kipotoshi A “udanganyifu” kilichaguliwa kwa asilimia 31.58 ambayo ni kubwa zaidi

kuliko majibu mengine yote kwasababu kina mfanano mkubwa na dhana ya neno “hila”. Hata hivyo swali liliwataka watambue kinyume chake na si kuchagua neno la kufanana. Kipotoshi B, D na E vilichaguliwa kutokana na uelewa mdogo wa watahiniwa kuhusu maana za misamiati.

**Swali la 39**: Neno “dalali” kama lilivyotumika katika habari hii lina maana gani?

A. Wakili
B. Mnadi
C. Mkopeshaji
D. Muuzaji
E. Mnunuzi.

Majibu ya watahiniwa

| Chaguo | A | B* | C | D | E | Wasiojibu | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya watahiniwa** | 124,883 | 199,890 | 140,065 | 214,026 | 177,893 | 5,109 | 3,240 |
| **Asilimia ya watahiniwa** | 14.44 | 23.11 | 16.19 | 24.74 | 20.56 | 0.59 | 0.37 |

Swali lilikuwa linapima matumizi ya misamiati kama ilivyotumika katika habari. Asilimia 23.11 ya watahiniwa walijibu kwa usahihi kwa kuchagua jibu B “Mnadi” ambalo lilikuwa tofauti kabisa na vipotoshi vilivyotolewa. Aidha watahiniwa waliochagua vipotoshi A, C, D na E walishindwa kumtofautisha mtu asiyekuwa na mali yake (dalali) na yule mwenye mali yake. Aidha walishindwa kutofautisha maana ya “wakili” anayemtetea mtu mahakamani; “mkopeshaji” wa hela; “muuzaji” wa mali ili apate hela; na “mnunuzi” anayetumia hela ili kupata mali.

**Swali la 40**: Funzo muhimu zaidi ulilolipata katika habari uliyosoma linawakilishwa na methali ipi?

A. Mali bila daftari hupotea bila habari
B. Biashara haigombi
C. Baniani mbaya kiatu chake dawa
D. Banda likikushinda jenga kibanda
E. Haba na haba, hujaza kibaba.

Majibu ya watahiniwa

| Chaguo | A* | B | C | D | E | Wasiojibu | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Idadi ya watahiniwa | 548,595 | 83,585 | 92,367 | 54,530 | 78,444 | 4,245 | 3,340 |
| Asilimia ya watahiniwa | 63.41 | 9.66 | 10.68 | 6.3 | 9.07 | 0.49 | 0.39 |

Swali lilikuwa linapima tathmini ya uelewa wa watahiniwa kuhusu mafunzo yatokanayo na methali. Asilimia 63.41 ya watahiniwa walielewa habari na kuweza kulinganisha funzo litokanalo na habari hiyo kuwa ni ‘A’ “Mali bila daftari hupotea bila habari”. Aidha, kipotoshi “C” kilichaguliwa kwa asilimia 10.68 kwa kuwa methali hii “Baniani mbaya kiatu chake dawa” ilionekana kuwa tofauti na methali nyingine zilizotolewa ambazo zilikuwa na dhana ya uzalishaji ndani yake au biashara.

## 2.4 Sehemu D: Ushairi

Katika sehemu hii watahiniwa walitakiwa kusoma shairi lililotolewa na kujibu maswali yanayotokana na shairi hilo.

*Wanafunzi sikiliza, nawapa huu wasia,*
*Nataka kuwaeleza, mambo muhimu sikia,*
*Kwanza ninawapongeza, hapa mlipofikia,*
*Hongereni hongereni, hongereni kuhitimu.*

*Hapa mlipofikia, kamwe msije bweteka,*
*Malengo kuyafikia, huu ni mwanzo hakika,*
*Usije kuvizikia, vitabuvyo kwenye taka,*
*Hongereni hongereni, hongereni kuhitimu.*

*Shuleni mmejifunza, masomo kwa uhakika,*
*Kiswahili ni cha kwanza, lugha hamkuichoka,*
*Kwa ari mkijifunza, mbele kitawapeleka,*
*Hongereni hongereni, hongereni kuhitimu.*

*Safari miaka saba, yenye raha na karaha,*
*Mlichopata si haba, mwende nacho kwa furaha,*
*Hicho kidogo kibaba, kisilete majeraha,*
*Hongereni hongereni, hongereni kuhitimu.*

**Swali la 41**: Mshairi anaposema “mlichokipata si haba” ana maana gani?

A. Mlichokipata si kilele
B. Mlichokipata si kidogo
C. Mlichokipata si duni
D. Mlichokipata si dhaifu
E. Mlichokipata si kibaya.

Majibu ya watahiniwa

| Chaguo | A | B* | C | D | E | Wasiojibu | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Idadi ya watahiniwa | 80,865 | 472,093 | 99,215 | 63,314 | 141,984 | 4,368 | 3,267 |
| Asilimia ya watahiniwa | 9.35 | 54.57 | 11.47 | 7.32 | 16.41 | 0.5 | 0.38 |

Swali lilikuwa linapima uelewa wa mtahiniwa kuhusu usomaji wa makini wa shairi. Asilimia 54.57 ya watahiniwa walijibu swali kwa usahihi kwa kuchagua jibu B kwa kuwa neno “haba” liliwawezesha kutambua jibu kwa urahisi kuwa ni ‘kidogo’ ambapo majibu ya vipotoshi A, C, D na E vilivyochaguliwa na watahiniwa kwa asilimia 44.55 vilionesha kuwa watahiniwa hao walikuwa hawana ujuzi wa kutosha kuhusu maana ya misamiati mbalimbali.

**Swali la 42:** Vina katika ubeti wa pili ni vipi?

A. ha na ka
B. a na ka
C. ho na ho
D. ni na mu
E. u na vi.

Majibu ya watahiniwa

| Chaguo | A | B* | C | D | E | Wasiojibu | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Idadi ya watahiniwa | 141,959 | 455,071 | 115,744 | 90,573 | 52,922 | 5,879 | 2,958 |
| Asilimia ya watahiniwa | 16.41 | 52.6 | 13.38 | 10.47 | 6.12 | 0.68 | 0.34 |

Swali lilikuwa linapima maarifa ya mtahiniwa kuhusu kanuni za utunzi wa shairi. Asilimia 52.6 ya watahiniwa walijibu swali kwa usahihi kwa kuchagua jibu B kwa kuwa walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu mbinu za utunzi wa mashairi kama vina vya shairi ambavyo ni **‘a’** na **‘ka’** vilivyojitokeza katikati na mwisho wa mstari. Watahiniwa waliochagua vipotoshi A, C, D na E walikosa ujuzi wa kuvijua vina vya shairi kwa kuzingatia kanuni ya utunzi wa shairi.

**Swali la 43**: Wazo kuu katika shairi hili ni lipi?

A. Kuhitimu ni jambo muhimu
B. Elimu ya msingi ni bora zaidi
C. Kujiendeleza kielimu ni muhimu
D. Kiswahili ni somo la muhimu
E. Kuhitimu ni lazima.

Majibu ya watahiniwa

| Chaguo | A | B | C* | D | E | Wasiojibu | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Idadi ya watahiniwa | 173,121 | 141,395 | 346,966 | 126,463 | 68,703 | 5,555 | 2,903 |
| Asilimia ya watahiniwa | 20.01 | 16.34 | 40.11 | 14.62 | 7.94 | 0.64 | 0.34 |

Swali lilikuwa linapima uelewa wa mtahiniwa kuhusu dhana nzima ya ushairi. Asilimia 40.11 waliweza kujibu swali kwa usahihi kwa kuchagua jibu C kwakuwa walikuwa na uelewa wa kutosha kuhusu lugha na mbinu za ushairi katika kupata ujumbe. Aidha watahiniwa waliochagua vipotoshi A, B, D na E walikosa ujuzi wa jinsi ya kupata maudhui katika utanzu wa ushairi. Hata hivyo kipotoshi A kilichaguliwa na asilimia 20.01 ya watahiniwa ambao ni wengi zaidi kuliko waliochagua vipotoshi vingine vyote kwa kuwa watahiniwa waliona ni muhimu kuhitimu na huenda wao wenyewe walikuwa wanafurahia kuhitimu elimu ya msingi.

**Swali la 44**: Kichwa kinachofaa kwa shairi hili ni kipi?

A. Ushauri kwa wahitimu
B. Kuhitimu ni fahari
C. Elimu ya msingi
D. Wanafunzi wahitimu
E. Fahari ya kuhitimu.

Majibu ya watahiniwa

| Chaguo | A* | B | C | D | E | Wasiojibu | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Idadi ya watahiniwa | 292,853 | 109,136 | 205,662 | 172,306 | 76,777 | 5,322 | 3,050 |
| Asilimia ya watahiniwa | 33.85 | 12.62 | 23.77 | 19.92 | 8.87 | 0.62 | 0.35 |

Swali lilikuwa linampima mtahiniwa kuhusu uelewa wa maudhui au ujumbe wa shairi kwa ujumla. Asilimia 33.85 walijibu swali kwa usahihi kwa

kubaini kichwa cha habari kuwa ni A “Ushauri kwa wahitimu.” Watahiniwa waliochagua vipotoshi B hadi E walikosa uelewa utokanao na usomaji wa shairi kwa makini. Aidha uchaguzi wa kipotoshi “C” kwa asilimia 23.77 umetokana na hatua ya elimu waliyoifikia watahiniwa hao.

**Swali la 45**: Kinyume cha neno “karaha” ni kipi?

A. Kero
B. Adabu
C. Furaha
D. Adhabu
E. Amani.

Majibu ya watahiniwa

| Chaguo | A | B | C* | D | E | Wasiojibu | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya watahiniwa** | 249,956 | 88,923 | 339,120 | 76,792 | 102,286 | 4,931 | 3,098 |
| **Asilimia ya watahiniwa** | 28.89 | 10.28 | 39.2 | 8.88 | 11.82 | 0.57 | 0.36 |

Swali lilikuwa linapima maarifa ya mtahiniwa kuhusu dhana zenye kutofautiana. Asilimia 39.2 ya watahiniwa walijibu swali kwa usahihi kwa kuwa dhana hiyo ilitofautiana waziwazi na majibu ya vipotoshi vilivyotolewa kulingana na maana ya kila moja. Asilimia 28.89 ya watahiniwa walichagua kipotoshi A “Kero” kwa kuwa hawakuzingatia kinyume cha neno “karaha” badala yake waliandika kisawe cha neno hilo. Kwa ujumla watahiniwa walikosa maarifa kuhusu maana za vipotoshi hivyo na maana halisi ya neno “Karaha”.

**Swali la 46**: Neno “bweteka” kama lilivyotumika kwenye shairi hilo lina maana ipi?

A. Kuridhika
B. Kudhihaki
C. Kudhoofika
D. Kudhalilika
E. Kudhihirika.

Majibu ya watahiniwa

| Chaguo | A* | B | C | D | E | Wasiojibu | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Idadi ya watahiniwa | 305,878 | 108,968 | 258,616 | 117,669 | 64,896 | 5,527 | 3,552 |
| Asilimia ya watahiniwa | 35.36 | 12.6 | 29.89 | 13.6 | 7.5 | 0.64 | 0.41 |

Swali lilikuwa linapima uelewa wa mtahiniwa kuhusu msamiati uliotumika katika shairi. Asilimia 35.36 walikuwa na uelewa wa msamiati uliotumika katika shairi, hivyo waliweza kuchagua jibu sahihi ambalo lilikuwa A. Watahiniwa waliochagua kipotoshi B - E ni asilimia 63.59 ambao walishindwa kujua kwamba maana ya neno "bweteka" si dhihaka, wala kudhoofika, kudhalilika au kudhihirika.

## 2.5 Sehemu E: Utungaji

Katika sehemu hii, watahiniwa walipewa habari yenye sentensi nne (4) zilizoandikwa bila mtiririko sahihi na walitakiwa wazipange sentensi hizo ili ziwe na mtiririko wenye mantiki kwa kuzipa herufi A, B, C na D.

**Swali la 47:** Dakika chache baadaye, tuliona msafara wa magari ukiingia

**Swali la 48:** Gari hilo lilifuatwa na gari lingine lililojaa askari wa kuzuia fujo, kisha lilifuata gari la Rais.

**Swali la 49:** Mnamo saa saba hivi tuliona pikipiki ya askari wa usalama barabarani ikija mbio kama mshale.

**Swali la 50:** Mbele ya msafara huo kulikuwa na pikipiki nne zilizofuatiwa na gari la polisi lenye king'ora.

Majibu ya watahiniwa

| Swali | Jibu sahihi | Idadi ya watahiniwa | Asimilia ya watahiniwa | % wasiojibu | % mengine | % Jibu E |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 47 | B | 392,116 | 45.33 | 0.52 | 0.35 | 3.51 |
| 48 | D | 366,615 | 42.38 | 0.51 | 0.37 | 4 |
| 49 | A | 494,848 | 57.2 | 0.45 | 0.35 | 3.97 |
| 50 | C | 352,556 | 40.75 | 0.36 | 0.28 | 4.7 |

Swali hili lililenga kupima uwezo wa watahiniwa katika upangaji wa mawazo katika mtiririko wenye mantiki. Zaidi ya nusu ya watahiniwa ambao ni asilimia 57.2 waliweza kuandika sentensi ya kwanza kwa usahihi kama ilivyotakiwa. Hata hivyo asilimia ilipungua katika upangaji wa sentensi ya pili kwani ni asilimia 45.33 ndiyo walioandika sentensi hiyo kwa usahihi. Katika kukamilisha sentensi mbili za mwisho asilimia ya watahiniwa ilipungua zaidi hadi kufikia asilimia 40.75 kwa sentensi ya tatu na 42.38 kwa sentensi ya nne. Asilimia 0.35 hadi 0.37 walijibu maswali haya kama yale ya kuchagua kwa kujaza kipengele E ambacho hakikuwepo katika sehemu hii ya mtihani. Watahiniwa hawa hawakuelewa maelekezo ya swali na pia inaelekea kuwa walikuwa wanachagua majibu bila kusoma kilichoandikwa kwani wangekuwa wanasoma wangebaini kuwa herufi E haikuwa miongoni mwa herufi walizopaswa kuziandika katika swali hilo.

## 3.0 HITIMISHO

Uchambuzi wa namna watahiniwa walivyojibu maswali unaonesha changamoto mbalimbali ambazo watahiniwa walikumbana nazo walipokuwa wakifanya mtihani. Idadi kubwa ya watahiniwa ilionesha kutokuwa na maarifa ya kutosha kuhusu matumizi sahihi ya sarufi ya lugha ya Kiswahili kama vile aina za maneno, upatanisho wa kisarufi, njeo na kauli mbalimbali za vitenzi vya Kiswahili. Aidha baadhi ya watahiniwa walionekana kukosa maarifa kuhusu uelewa wa misamiati ya Kiswahili, utambuzi wa misemo na semi mbalimbali za Kiswahili kama vile methali, nahau na vitendawili; utungaji na ushairi wa Kiswahili.

Kutokana na uchambuzi huu, inaonesha wazi kuwa suala la ujifunzaji na ufundishaji wa somo la Kiswahili kwa shule za msingi linatakiwa lifanyike kwa ukamilifu ili kuwawezesha wanafunzi kutumia Kiswahili fasaha. Kwa kupitia wadau mbalimbali wa lugha ya Kiswahili, somo hili linatakiwa kupewa kipaumbele kwa kuwawezesha wanafunzi kupata maarifa ya kutosha kuhusu somo la Kiswahili ili waweze kukabiliana na changamoto mbalimbali za kitaaluma na za kimaisha kuhusiana na lugha ya Kiswahili.

Itambulike wazi kuwa Kiswahili ni lugha ya Taifa, ni sehemu ya utamaduni wa Mtanzania na ni lugha inayotegemewa katika kuziunganisha nchi za Jumuiya ya Afrika ya Mashariki na pia hutumika kimataifa. Hivyo, ni vema juhudi endelevu za kuinua lugha hii zifanyike kuanzia shule za msingi hadi elimu ya juu. Kwa kufanya hivi, lugha hii ya Kiswahili itakuwa imetendewa haki na kupewa hadhi inayostahili katika taifa hili.

## 4.0 MAONI NA MAPENDEKEZO

Ili kuwawezesha watahiniwa kupata maarifa na ujuzi wa kutosha na pia katika kuboresha matokeo yao katika mtihani wa Kiswahili mambo yafuatayo hayana budi kuzingatiwa:

(a) Mamlaka husika zihakikishe kuwa shule zote za msingi zinakuwa na vitabu vya kiada na vya ziada vya kutosha kwa ajili ya somo la Kiswahili.

(b) Walimu wanaofundisha somo la Kiswahili katika shule za msingi wanatakiwa kufundisha mada zote kwa ukamilifu kama ilivyoelekezwa katika muhtasari.

(c) Ili kupata ujifunzaji na ufundishaji wenye mafanikio, walimu wanatakiwa kutoa mazoezi ya kutosha kwa wanafunzi kuhusiana na mada mbalimbali wanazofundisha, ikiwa ni pamoja na kuwapa wanafunzi mrejeo wa matokeo ya mazoezi hayo kila mara.

(d) Wanafunzi wajengwe kifikra kuhusiana na umuhimu wa somo la Kiswahili katika maisha yao ili waweze kuondoa dhana iliyojengeka kwa wengi ya kuliona somo la Kiswahili kama somo lisilo na tija kwao kwa maisha ya baadaye.

(e) Wanafunzi wahamasishwe katika kutumia Kiswahili sanifu katika mazungumzo na maandishi yao ya kila siku ili kuboresha misamiati na sarufi ya lugha ya Kiswahili kwa ujumla.

CYMK